**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA NNE

**21 APRILI, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 21 APRILI, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**114. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga na kukarabati majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Mbinga kutokana na kukosa baadhi ya majengo na yaliyopo kuchakaa.

**115. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini barabara ya kutoka Kilando – Katete – Kazovu – Korongwe katika Wilaya ya Nkasi itakamilika.

**116. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza maelekezo ya Mhe. Waziri Mkuu ya ujenzi wa barabara ya urefu wa Km 5 kwa kiwango cha lami Wilayani Ikungi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**117. MHESHIMIWA ABDALLA RASHID RASHID (KIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali itajenga tuta kuzuia maji ya Bahari ya Hindi yasiathiri mashamba na mazao ya Wakulima wa Vijiji vya Nanguji, Jundamiti, Mwambe na Kiwani.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**118. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

(a) Je, ni nini sababu ya kuweka tozo ya ada ya tathmini ya asilimia moja kwa mkopaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambapo asilimia 50 inalipwa kabla ya kuanza kufanya tathmini na asilimia 50 inalipwa baada ya mkopo kuidhinishwa;

(b) Je, ni kigezo gani kilipelekea tozo kuwa asilimia 1 na si vinginevyo;

(c) Je, mkopo usipoidhinishwa hiyo asilimia 50 ya asilimia 1 iliyolipwa inarudishwa ama la.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**119. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Chuo cha VETA Shaurimoyo – Ludewa ili kuzalisha Wataalam watakaosaidia kutekeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma utakapoanza.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**120. MHESHIMIWA SILLO DANIEL BARAN (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Dareda – Bashnet – Dongobesh kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**121. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

(a) Je, Serikali inawatumia vipi Wanafunzi wanaohitimu Shahada ya *Science Industrial Engineering Management* katika uchumi huu wa kati na viwanda;

(b) Je, ni Wanafunzi wangapi waliohitimu katika fani hiyo wameajiriwa Serikalini tangu Mwaka 2019 – 2020.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**122. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itasomesha Wataalam wa *Court Reporting* na *Stenographer* ili Mahakama zetu ziwe na Wataalam hao.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**123. MHESHIMIWA MOHAMMED JUMAH SOUD (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Mifuko ya Kuendeleza Utalii na Wanyamapori na kufikia lengo la Watalii milioni tano ifikapo Mwaka 2025.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**21 APRILI, 2021** **KATIBU WA BUNGE**